KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 1

KANUNI ZA UONGOZI NA MAADILI

Toleo la Februari, 2010

Zimetolewa na:
Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM

Bei Sh.500/=

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 2

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 3

CHAMA CHA MAPINDUZI

KANUNI ZA UONGOZI NA MAADILI

TOLEO LA FEBRUARI, 2010

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 4

Madhumuni na lengo Kuu la CCM ni hili:

(KATIBA YA CCM 1977 TOLEO LA 2010)

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 5

YALIYOMO

1 UTANGULIZI 1

(i) Katiba ya Chama Cha Mapinduzi..... 2
(ii) Sera za Chama Cha Mapinduzi 2
(iii) Kadi za Chama Cha Mapinduzi 3
(iv) Jukumu la Kiongozi wa Chama Cha Mapinduzi 4

2 FUNGU LA KWANZA

Muundo wa Kamati za Usalama na Maadili … 5

3. FUNGU LA PILI

Majukumu ya Kamati ya Usalama na Maadili.. 8

3 FUNGU LA TATU

(i) Wajibu wa kusimamia Tabia, Mwenendo na Vitendo vya Mwanachama na Kiongozi 13
(ii) Maadili ya Wanachama 16
(iii) Mambo yasiyoruhusiwa 17

4 FUNGU LA NNE

(i) Taratibu za kushughulikia Maadili 23
(ii) Adhabu 26
(iii) Utaratibu wa kuendesha Vikao 33
(iv) Kubadili Kanuni 41

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 6

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 7

1. UTANGULIZI

i. Tangu mwanzo Vyama vya TANU na ASP, kwa kuzingatia umuhimu wa Umoja na Mshikamano wakati wa Mapambano, vilikuwa na taratibu za kudumisha Maadili ya Wanachama wao, kuwarekebisha wanaorekebishika, au kuwaondoa katika Chama wale wanaoonekana kuwa ni mzigo. Hazikuweko Kanuni zilizoandikwa, lakini Wanachama walionywa na wengine walitoswa, ili kulinda na kudumisha mshikamano ulioleta Uhuru.

Hali iliendelea hivyo mpaka baada ya kuunganisha TANU na ASP na kuundwa CCM na pale Mwongozo wa Chama (1981) ulipobaini umuhimu wa Chama kujiunda upya ili kuongoza Mapinduzi. Halmashauri Kuu ya Taifa iliaunda Tume ya Udhibiti na Nidhamu ili kuisaidia kutekeleza wajibu wake wa Katiba wa kusimamia Maadili ya Wanachama na Viongozi, hasa kwa lengo la kuwaepusha kuvunja Miiko ya Uongozi ya Azimio la Arusha.

ii. Baada ya Miiko ya Azimio la Arusha kupewa tafsiri pana zaidi, kutokana na kuingia kwa Mfumo wa Vyama vingi, ilionekana kuwa Tume ya Udhibiti na Nidhamu katika sura ile iliyokuwa nayo isingeoana na mazingira hayo mapya, ambapo CCM yenyewe ilitakiwa kusimamia Mageuzi. Lakini, kwa kuwa Maadili na Mshikamano ni muhimu zaidi sasa kuliko ilivyokuwa wakati wa Chama kimoja huko nyuma, kilibakizwa Kitengo cha kusimamia Maadili.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 8

iii. Shabaha ya Kanuni hizi ni kuweka Taratibu zitakazotumiwa na Kamati za Usalama na Maadili katika kufanya kazi zake za kusimamia Katiba ya CCM, Sera za Chama, Kanuni na Taratibu zote za Chama zilizowekwa kuongoza ustawi wa Chama cha Mapinduzi.

iv. **Katiba ya Chama Cha Mapinduzi**

Katiba ya Chama ndio sheria kuu ya Chama Cha Mapinduzi inayoonyesha organaizesheni ya chama, Malengo na Madhumini ya Chama. Vilevile inaainisha Haki Wajibu wa Mwanachama; Sifa, Miiko, Majukumu ya Utendaji, Uongozi na Vikao vya Chama. Utekelezaji wa katiba ya CCM umefafanuliwa pia katika Kanuni mbalimbali za Chama kama zilivyotolewa na kusimamiwa na Halmashauri Kuu ya Taifa. Kufuata na kutii Katiba ya CCM na Kanuni zake ni wajibu wa kila mwanachama wa CCM.

v. **Sera za Chama Cha Mapinduzi**

Sera za Chama cha Mapinduzi ni Dira ya kuongoza umma wa Watanzania katika ujenzi wa uchumi wa kisasa utakaoleta maisha bora ya wananchi kwa kuwawezesha kiuchumi kama inavyoainishwa katika Ilani ya uchaguzi ya Chama. Utekelezaji mzuri wa sera utakijengea sifa Chama na kukifanya kikubalike zaidi kwa wanachi. Lakini wenye sera zao ni wanachama ndio wanaotarajiwa kuzilinda na kuzitetea, na kuhimiza utekelezaji wake.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 9

Kwa hali ilivyo sasa unahitajiwa umoja wa nguvu zaidi katika kutetea sera za Chama, ambazo lazima zinapingwa na vyama vingine. Huko nyuma tumeona hata baadhi ya wanachama wakipinga hadharani Sera za CCM. Kamati ya Usalama na Maadili sasa italazimika kushughulikia usaliti wa aina hii.

vi **Kadi za Chama Cha Mapinduzi ni mali ya CCM**

(a) Kadi ya CCM ni alama ya Uanachama wa Chama Cha Mapinduzi. Atakayejiunga au kuwa mwanachama wa CCM atapewa au atakuwa na kadi ya Chama Cha Mapinduzi. Mtu ye yote ambaye uanachama wake utakwisha kwa mujibu wa ibara ya 13(1) ya Katiba (1977) atalazimika kurudisha Kadi yake ya CCM kwenye Tawi alikoipata.

(b) Mwangalizi wa Mirathi wa marehemu aliyekuwa mwanachama wa CCM atalazimika kurudisha kadi ya marehemu pale marehemu alipoipata.

(c) Katibu wa Tawi atakayepokea Kadi ya mtu ambaye uanachama wake umekwisha kwa mujibu wa ibara 13(1) ya Katiba ya CCM 1977 au kadi ya marehemu aliyekuwa mwanachama, atatakiwa kuthibitisha kwa maandishi kuipokea kadi hiyo na kumfuta mwenye kadi kwenye daftari la orodha ya wanachama.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 10

(vii) **Jukumu la Kiongozi wa CCM**

Maadili ya Kiongozi yakitetereka, Chama kitavurugika na nchi itakwenda mrama. Hivyo jukumu la kiongozi litakuwa:-

(a) Kukijenga na kukilinda Chama.
(b) Kuwa na Maadili mema na kutotenda maovu.
(c) Kutimiza wajibu wake kwa ukamilifu.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 11

FUNGU LA KWANZA

MUUNDO WA KAMATI YA USALAMA NA MAADILI

2. (1) Ni dhahiri kwamba kazi za Kamati za Usalama na Maadili zitakuwa muhimu sana katika kipindi hiki, na kwamba kazi hizo zitaongezeka. Lakini haitawezekana kuzisimamia kwa ufanisi kazi zote hizi kutoka Makao Makuu; lazima usimamizi wa Maadili ufanywe na kila ngazi ya uongozi kutoka Taifa hadi Tawi la CCM.

(2) Kwa hiyo Kamati za Usalama na Maadili zitaundwa katika kila Ngazi, na kwa jinsi kazi zenyewe zilivyo, Kamati hizo lazima ziwe ndogo ili kutunza siri. Kwa hiyo Muundo wa Kamati hizo utakuwa ufuatao:-

(i) **Ngazi ya Taifa**

(a) Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Makamu wawili wa Mwenyekiti wa CCM CCM – Wajumbe
(c) Katibu Mkuu wa CCM - Katibu
(d) Makamu wa Rais – Mjumbe
(e) Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara na Zanzibar - Wajumbe
(f) Wajumbe wanne wa Kamati Kuu, wawili kutoka Bara na wawili kutoka Zanzibar , (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(ii) **Zanzibar**

(a) Makamu Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Naibu Katibu Mkuu wa CCM - Katibu
(c) Waziri Kiongozi anayetokana na CCM – Mjumbe
(d) Wajumbe watatu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(iii) **Ngazi ya Mkoa**

(a) Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM - Katibu
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(iv) **Ngazi ya Wilaya**

(a) Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM - Katibu
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(v) **Ngazi ya Jimbo**

(a) Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM – Katibu.
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(vi) **Ngazi za Kata/Wadi**

(a) Mwenyekiti wa CCM – Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM – Katibu

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 13

(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (Jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(vii) **Ngazi ya Tawi**

(a) Mwenyekiti wa CCM - Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM - Katibu
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 14

FUNGU LA PILI

MAJUKUMU YA KAMATI YA USALAMA NA MAADILI

3. (1) Kikao chenye jukumu la Kikatiba la kusimamia mwenendo mzima wa Nidhamu ya Chama ni Halmashauri Kuu Taifa. Lakini Madaraka ya utekelezaji yamo mikononi mwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(2) Kwa hiyo wajibu wa Kamati ya Usalama na Maadili ya kila ngazi ya Uongozi wa Chama ni kuiwezesha Kamati Kuu kutekeleza kwa ufanisi zaidi kazi zake za siku kwa siku za kusimamia Nidhamu ya Wanachama na Viongozi wa CCM ndani ya mfumo wa Vyama Vingi. Kamati Kuu ndiyo itakayoamua jambo gani lifikishwe Halmashauri Kuu ya Taifa, na lifikishwe namna gani.

(3) Kazi za Kamati hiyo katika kila Ngazi zitakuwa zifuatazo:-

(i) Kutoa ushauri kwa Kamati ya Siasa inayohusika kuhusu:-

(a) Masuala ya Usalama na Maadili katika Chama Cha Mapinduzi. Katika hili hakuna mipaka, kwa sababu masuala haya ya Usalama na Maadili huzuka mahali popote katika ngazi za uongozi wa Chama.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 15

(b) Kuweka Mikakati na Mbinu ya kuwalinda Viongozi wa CCM, Vikao vya Chama, Mikutano ya Hadhara na Ofisi za Chama.

(ii) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Maagizo na Maamuzi ya Usalama na Maadili ya Kamati ya Chama inayohusika

(iii) Kubuni mbinu za kuwashirikisha wanachama wa CCM na Viongozi katika Ngazi inayohusika katika mikakati ya Ulinzi na Usalama.

(iv) Kuchambua na kuainisha mbinu, hila na uwezo wa wapinzani na maadui wa CCM katika ngazi inayohusika, na kuweka mikakati ya kukabiliana nao.

(v) Kusimamia ipasavyo Maadili ya Wanachama, Viongozi na Vikao vyao, kulingana na Haki, Wajibu, Imani na Masharti ya Wanachama wa CCM.

(vi) Kila ngazi itawasilisha Taarifa yake, kila mwezi kwa ngazi ya juu yake, isipokuwa kama linatokea jambo kubwa ambalo haliwezi kusubiri utaratibu huo.

(vii) Kwa sababu hiyo, Kamati za Usalama na Maadili zitachambua kwa makini ubora wa Wanachama wanaoomba Uongozi, ama Viongozi wanaoteuliwa katika ngazi mbali mbali za Chama, kabla Vikao vinavyohusika havijatoa idhini ya kuwaruhusu wateuliwe kugombea uongozi huo wateuliwe kushika nafasi zilizo kusudiwa.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 16

(4) **Kamati za Udhibiti**

(i) Kutakuwa na Kamati Ndogo ya Udhibiti ya Kamati ya Usalama na Maadili kwa ngazi za Wilaya hadi Taifa itakayokuwa na Wajibu wa kusikiliza, kuhoji na kupendekeza adhabu kwa watuhumiwa wenye mashitaka yatakayopelekwa kwa uamuzi kwenye vikao vya ngazi hizo.

(ii) **Kamati Ndogo ya Udhibiti Ngazi ya Taifa itakuwa na wajumbe 4:**

(a) Makamu Mwenyekiti (Bara), - Mwenyekiti

(b) Mkurugenzi wa Maadili Ngazi ya Taifa, - Katibu

(c) Wajumbe wawili wanaoteuliwa na Kamati Kuu kutoka miongoni mwa wajumbe wake, mjumbe mmoja atoke upande wa Tanzania Bara na mjumbe wa pili atoke upande wa Zanzibar.

(d) Katika nyakati ambapo Kamati hii itakuwa ikifanya kazi zake mikoani, itakuwa na Wajumbe wawili zaidi ambao ni Wazee/Waasisi wawili wa Mkoa husika walioteuliwa kwa madhumuni hayo.

(iii) **Kamati Ndogo ya Udhibiti ya Mkoa:**

(a) Mwenyekiti wa Mkoa, - Mwenyekiti
(b) Afisa Maadili Mkoa, - Katibu
(c) Wazee / Waasisi 2, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 17

(iv) **Kamati Ndogo ya Udhibiti ya Wilaya**

(a) Mwenyekiti wa Wilaya, - Mwenyekiti
(b) Afisa Maadili Wilaya, - Katibu
(c) Wazee/Waasisi 2, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(v) **Kamati Ndogo ya Udhibiti ya Jimbo**

(a) Mwenyekiti wa CCM – Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM – Katibu
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(vi) **Kamati Ndogo ya Udhibiti ya Kata/Wadi**

(a) Mwenyekiti wa CCM – Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM – Katibu.
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

(vii) **Kamati Ndogo ya Uthibiti ya Tawi**

(a) Mwenyekiti wa CCM – Mwenyekiti.
(b) Katibu wa CCM – Katibu
(c) Wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa, (jinsia ikizingatiwa) - Wajumbe.

Kamati za Usalama na Maadili za Ngazi hizo zitafanya pia kazi hiyo ya udhibiti.

(viii) **Kamati ya Usalama na Maadili, kupitia Kamati yake Ndogo itakuwa na uwezo wa :-**

(1) Kumhoji Mwanachama au Kiongozi ye yote wa CCM , ama kujibu Tuhuma, ama kutoa Taarifa, zitakazosaidia kufafanua suala lenye utata.

(2) Kupata nyaraka au kumbukumbu zo zote zinazohitajika katika kutekeleza kazi hizo. Hatimaye Nyaraka hizo zitarudishwa salama pale zilipopatikana.

(5) **Majukumu Maalum ya Kamati ya Ngazi ya Taifa**

(i) Kuhakikisha kwamba shughuli za Chama zinaendeshwa kwa nidhamu ya hali ya juu, kwa kuzingatia wakati wote kuwa tuko katika Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa.

(ii) Kuendeleza moyo wa kuwajibika miongoni mwa Viongozi wa CCM.

(iii) Kufanya majumuisho ya Hali ya Siasa kwa nchi nzima, na kupendekeza kwa Kamati Kuu hatua za kuchukua.

(iii) Kamati ya Usalama na Maadili itasikiliza malalamiko ya Rufaa za wanachama waliokwisha kuteuliwa kushindania kiti cho chote cha uongozi wa Chama, endapo wanachama hao wanaamini kuwa Uchaguzi huo umeendeshwa kinyume cha Kanuni, na kupendekeza kwa kikao cha Kamati ya Siasa ya ngazi inayohusika au cha Kamati Kuu kwa kutolewa uamuzi unaopasa.

Kazi za Kamati za Maadili zitafuatiliwa na kuratibiwa na Kitengo cha Maadili ya Viongozi na Wanachama kilichopo chini ya Ofisi ya Katibu Mkuu.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 19

FUNGU LA TATU

WAJIBU WA KUSIMAMIA TABIA, MWENENDO NA VITENDO VYA MWANACHAMA NA KIONGOZI

4. Wajibu wa kusimamia Tabia, Mwenendo na Vitendo vya Mwanachama na Kiongozi ni wa vikao vya Chama Cha Mapinduzi kwa mujibu wa Katiba ya Chama kama ifuatavyo:

(1) **Halmashauri Kuu ya Tawi**

Ibara ya 37(5):-

Kuangalia mwenendo na vitendo vya Wanachama na Viongozi wa CCM katika Tawi na inapolazimu kutoa Taarifa kwa vikao vya CCM vinavyohusika.

(2) **Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi**

Ibara ya 47 (7), (12):-
(7) Kuangalia mwenendo na vitendo vya Wanachama pamoja na viongozi wa CCM, na inapolazimu kutoa Taarifa kwa vikao husika.

(12) Kumsimamisha Uanachama Mwanachama yeyote ambaye mwenendo na tabia yake vinamwondolea sifa za Uanachama.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 20

(3) **Kamati ya Siasa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi**

Ibara ya 53(5):-
Kumsimamisha uongozi kiongozi ye yote wa ngazi ya Tawi au Shina, endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa ya uongozi.

(4) **Halmashauri Kuu ya Jimbo (Zanzibar)**

Ibara ya 51(7):-
Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama pamoja na viongozi wa CCM na inapolazimu kutoa Taarifa kwa vikao husika.

(5) **Halmashauri Kuu ya Wilaya**

Ibara ya 79(7):-
Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama pamoja na viongozi wa CCM katika Wilaya na inapolazimu, kutoa Taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(6) **Kamati ya Siasa ya Wilaya**

Ibara ya 81(7):-
Kumsimamisha uongozi kiongozi ye yote wa ngazi ya Kata/Wadi na Jimbo endapo itadhihirika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi.

(7) **Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa**

Ibara ya 93(8),(14) na (15):-

(8) Kuangalia mwenendo na vitendo vya Wanachama na Viongozi wa CCM katika Mkoa na inapolazimu kutoa Taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(14) Kumwachisha au kumfukuza uanachama mwanachama ye yote endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uanachama. Mwanachama anayeachishwa au kufukuzwa uanachama anaweza kukata rufaa kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(15) Kumwachisha au kumfukuza uongozi kiongozi ye yote ambaye uteuzi wake wa mwisho unafanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(8) **Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Mkoa**

Ibara ya (95)(7);

(7) Kumsimamisha uongozi kiongozi ye yote wa ngazi ya Wilaya endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi. Isipokuwa kwamba haitakuwa na uwezo wa kumsimamisha uongozi kiongozi ambaye uteuzi wake wa mwisho haukufanywa na Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa.

(9) **Halmashauri Kuu ya Taifa**

Ibara ya (107)(21) na (22):-

(21) Kumsimamisha Mwenyekiti wa CCM au Makamu wa Mwenyekiti wa CCM iwapo mwenendo au utendaji wake wa kazi vinamwondolea sifa za uongozi. Hata hivyo Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafikisha mapendekezo yake mbele ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(22) Kumwachisha au kumfukuza uongozi kiongozi ye yote ambaye uteuzi wake wa mwisho ulifanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(10) **Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa**

Ibara ya 109(7):-
Kumsimamisha uongozi kiongozi ye yote isipokuwa Mwenyekiti wa CCM na Makamu Mwenyekiti wa CCM endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake utamwondolea sifa za uongozi.

MAADILI YA WANACHAMA

5. (1) Kuhakikisha kuwa wanachama wanatimiza masharti ya uanachama wao, wajibu wao, na wanatekeleza ahadi za mwana CCM; na kujitahidi kuhakikisha kuwa haki za kila mwanachama hazivizwi.

(2) Kuhakikisha kuwa wanachama wanaovunja Maadili ya Chama kama yalivyoainishwa katika

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 23

Katiba ya CCM na Kanuni za CCM wanachukuliwa hatua za kuwarekebisha na kama itashindikana kuwarekebisha, kuwaondoa katika Chama au katika Uongozi.

MAMBO YASIYORUHUSIWA

6. (1) Katika kupambana na vitendo vya rushwa wakati wa chaguzi mbalimbali za Chama, Kiongozi ye yote atakayethibitika kuwa ameshinda uchaguzi kutokana na kitendo cho chote cha rushwa atanyang'anywa ushindi alioupata, na pia atazuiwa kugombea tena uchaguzi mwingine wo wote kwa muda utakaoamuliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(2). Kwa hiyo mwanachama haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuomba au kukusanya misaada au michango kwa ajili ya Chama au Jumuiya yake bila kwanza kupata idhini ya Kikao halali cha Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya ngazi inayohusika.

(ii) Kutoa michango, misaada au zawadi za vifaa au nyenzo kwa mtu au shughuli yeyote mpaka iwe tu kwa ridhaa ya Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya ngazi inayohusika, kwa masharti kwamba Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa inapata Taarifa.

(iii) Kutoa michango, misaada, zawadi, n.k, katika eneo ambako mwanachama huyo anakusudia

kugombea nafasi yo yote ya uongozi, na endapo katika mazingira maalum ruhusa imetolewa mchango huo kupokelewa kama ilivyofafanuliwa katika vifungu 6(2)(i) na 6(2) (ii) basi mchango huo hautatangazwa.

(iv) Kwa kufuata taratibu zilizoonyeshwa katika vifungu 6(2)(i) na 6(2) (ii). Viongozi wa kuchaguliwa wa Ngazi zote, wanaruhusiwa kutafuta michango/misaada kwa ajili ya shughuli za Chama au za Maendeleo ya Umma katika maeneo yao katika kipindi cho chote kisichokuwa cha uchaguzi; lakini miradi iliyokwisha anzishwa na viongozi waliopo madarakani itaruhusiwa kuendelea kuchangiwa hata katika kipindi cha uchaguzi.

(v) Mwanachama anayewania nafasi ya uongozi katika Chama au Jumuiya hataruhusiwa yeye mwenyewe au wakala wake, nje ya utaratibu uliowekwa, kutembelea Tawi, Kata/Wadi, Jimbo, Wilaya, Mkoa au Nchi nzima, kulingana na eneo analowania uongozi, akishawishi wanachama wenzake kwa ahadi, misaada, michango, tafrija, n.k. ili wampigie kura wakati utakapofika.

(3) **Haki na Wajibu wa mwanachama**

(i) Mwanachama atakuwa na haki ya kugombea nafasi ye yote ya Uongozi; lakini endapo kugombea nafasi nyingi kutasababisha kuzorota kwa uhai wa Chama, hatateuliwa.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 25

(ii) Mwanachama au Kiongozi wa CCM atakayekataa Maamuzi ya Kikao halali cha Chama atakuwa ametenda kosa la utovu wa nidhamu; na atadhibitiwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(iii) Mwanachama atakayekataa kumuunga mkono mgombea wa CCM aliyeteuliwa na Kikao halali cha Chama na akithubutu kufanya kampeni za siri au za wazi kumhujumu, atakuwa ametenda kosa la usaliti, na atastahili adhabu ya kufukuzwa uanachama.

(4) **Taratibu za kuomba Uongozi**

(i) Mwanachama anayegombea nafasi yo yote ya Uongozi wa Chama atapaswa kuchukua Fomu na kuirejesha pale anapofahamika tabia, mwenendo na mahusiano yake na watu, na jinsi anavyotekeleza Masharti ya Uanachama, Ahadi za Uanachama na Wajibu wa Uanachama wake.

(ii) Wanachama wanaogombea uongozi ambao uteuzi wao hufanywa na Vikao vya Kitaifa, watachunguzwa kwanza uadilifu wao na chombo cha Chama cha Maadili kwa ushirikiano na vyanzo vingine.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 26

(5) **Kuwanunulia watu Kadi**

Mwanachama ye yote wa CCM, anayegombea nafasi ya Uongozi wa Chama au wa Jumuiya, haruhusiwi kuwanunulia Kadi za CCM au za Jumuiya watu wengine kwa lengo la kuwawezesha kumpigia kura. Mgombea pia haruhusiwi kuwalipia ada wanachama wasio hai, ili awape haki ya kumpigia kura.

(6) **Takrima**

(i) Mwanachama ye yote anayegombea nafasi ya uongozi ndani ya Chama haruhusiwi kutoa takrima (kuwasafirisha, kuwapa malazi, chakula, vinywaji) Wajumbe wa Mkutano wa Uchaguzi wa ngazi anayogombea kinyume cha utaratibu uliowekwa na Kamati ya Siasa ya ngazi hiyo.

(7) **Kampeni**

(i) Wanachama wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi katika muhula unaofuata (Ubunge, Uwakilishi, Udiwani na nafasi nyingine katika Chama wanaweza kutangaza nia zao lakini hawaruhusiwi kufanya kampeni kabla ya muda uliowekwa rasmi. Muda wa kampeni unaanza baada ya majina ya wagombea kuteuliwa na kikao kinachohusika.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 27

(8) **Miiko Mingineyo**

(i) Msimamizi wa Uchaguzi na/au Wagombea nafasi za Uongozi watakaothibitika kushiriki katika vitendo vya rushwa watadhibitiwa na kupewa adhabu inayowastahili; na kama ni Wagombea, watapewa adhabu bila kujali kama wameshinda au wameshindwa.

(ii) Kiongozi ye yote wa CCM ataandika katika Fomu iliyoandaliwa kwa madhumuni hayo mali zote alizonazo, na jinsi alivyozipata, mara baada ya kuchaguliwa au kuteuliwa kushika Uongozi; na atafanya hivyo kila mwaka mpaka uongozi wake utakapokoma. Aidha, litakuwa kosa kubwa kwa kiongozi kukwepa kujaza Fomu hiyo, au kujaza kwa namna isiyobainisha mali zake zote; na kwa kosa hilo mtu anaweza kuvuliwa uongozi, au hata kunyang'anywa uanachama.

(iii) Ni mwiko kwa Kiongozi wa CCM kuwa na uhusiano wa karibu na mtu au kampuni yenye vitendo vilivyo kinyume na Maadili ya Chama au ya Taifa; k.m. wala rushwa, wakwepa kodi, wenye biashara za madawa ya kulevya n.k. Kwa kuvunja mwiko huo kiongozi atalazimika kujiuzulu uongozi wake.

(iv) Ni mwiko kwa kiongozi (ibara 18 (1) ya Katiba ya CCM) kutoa ama kupokea kutoka kwa mtu ye yote, jamaa zake, au wakala wa mtu huyo,

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 28

ahadi, zawadi, fedha, (takrima), n.k. ili mtu huyo ampendelee yeye katika kumfanikishia maslahi yake binafsi hasa uongozi.

(v) Ni mwiko kwa Kiongozi wa CCM kutumia dini yake au kabila au rangi au jinsia au eneo analotoka, kama sifa ya kushawishi wapiga kura wamchague ama yeye mwenyewe ama mgombea anayemuunga mkono. Kadhalika ni mwiko kwa Kiongozi kujenga au kudumisha makundi yenye sura hiyo yanayovuruga Umoja na Mshikamano ndani ya Chama.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 29

FUNGU LA NNE

TARATIBU ZA KUSHUGHULIKIA MAADILI

7. (1) Katika kusimamia maadili ya Viongozi wa CCM wakati wo wote wa utekelezaji wa Kanuni hizi, Kamati ya Usalama na Maadili katika ngazi inayohusika itazingatia Katiba ya CCM na Kanuni zingine za CCM zitakazokuwepo wakati huo pamoja na maelekezo mengine ya msingi yatakayokuwa yametolewa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(2) Mwanachama wa CCM anapoomba Uongozi katika Ngazi yo yote, itikadi na mwenendo wake vitachunguzwa kwanza na Kamati ya Usalama na Maadili inayohusika, ndipo maombi hayo yaliyoambatanishwa na mapendekezo ya Kamati ya Usalama na Maadili yatakapofikishwa mbele ya kikao chenye madaraka ya kutoa maamuzi.

(3) Ikiwa Mwanachama hakupendekezwa kwa sababu ya kukiuka Katiba ya CCM, Kanuni za CCM na Sheria ya nchi, Mwanachama huyo hatakuwa na haki ya kukata rufaa kwa mtu ye yote au kikao cho chote. Lakini ikiwa mwanachama atakataliwa kugombea kwa sababu ya madhambi yake katika Chama, basi ni wajibu wa Kamati ya Usalama na Maadili kumjulisha mwanachama huyo makosa yaliyomnyima haki ya kugombea, naye anaweza kukata rufaa kwa mujibu wa haki zake kikatiba.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 30

(4) **Tuhuma**

(i) Mtu ye yote anayetuhumiwa mbele ya Kamati ya Usalama na Maadili ya ngazi yo yote, kwa kosa lo lote linalohusiana na Maadili au Nidhamu ya Chama atasomewa na kutakiwa kuzijibu tuhuma hizo mbele ya Wajumbe wa Kamati hiyo ama kwa kauli yake mwenyewe ama kwa maandishi; lakini hataambiwa nani aliyezileta tuhuma hizo, isipokuwa kama imekwishajulikana mapema kutokana na mijadala ya vikao, vyombo vya sheria au vyombo vya habari.

(ii) Uchambuzi wa tuhuma hizo utafanywa kwa kutumia njia mbali mbali pamoja na mashahidi watakaoweza kupatikana. Uchunguzi utakapokamilika, na endapo itadhihirika kwamba tuhuma zina uzito, mtuhumiwa ataitwa mbele ya kikao cha Kamati ya Usalama na Maadili ya ngazi inayohusika, kama ni lazima, ili apate kuhojiwa ana kwa ana.

(iii) Kamati ya Usalama na Maadili ya ngazi inayohusika itatoa mapendekezo yake kuhusu suala hilo, kwenye kikao cha maamuzi kinachohusika. Mtuhumiwa atapewa nakala ya maamuzi kwa maandishi.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 31

(5) **Makosa ya Vikao vya CCM**

(i) Kosa la kikao katika masuala ya Maadili litakuwa na sura mbili: sura ya kutenda, au ya kutotenda. Kikao kitakachoazimia kukataa misingi ya Imani ya CCM na kuongeza uasi katika Chama, au kitakachoamua jambo kama kugomea michango halali ya wanachama, kitakuwa na kosa la uasi, na kitastahili adhabu itakayolingana na kosa lenyewe.

(ii) Kikao cho chote cha Chama hakiruhusiwi kuweka au kutangaza “Msimamo” kwa nafasi yo yote inayogombewa ndani ya Chama. Kufanya hivyo ni kuviza Haki za Wanachama wengine kwa mujibu wa Ibara ya 14(3) ya Katiba ya CCM.

(iii) Kikao chenye Wajibu wa Kikatiba wa kusimamia Tabia na Mwenendo wa Wanachama na Viongozi wanaokiuka makusudi Maadili ya Chama, lakini kinachelea kuwachukulia hatua kitakuwa kimefanya kosa la Kimaadili.

a. Kwa kawaida makosa kama hayo hutokana na uchochezi wa viongozi wachache. Kitengo kinapaswa kuchambua chimbuko la maamuzi kama hayo na kupendekeza namna ya kuling’oa hilo Shina la Uasi;maana likiachiliwa litaeneza uasi nchini kote na Chama hakitakuweko tena.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 32

(6) **Utunzaji wa Siri za Vikao**

Litakuwa ni kosa kubwa la Maadili kwa Kiongozi au Mjumbe wa Kikao cho chote cha Chama kutoa siri ya Kikao au Nyaraka za siri kwa watu wasiohusika.

ADHABU

8. (1) Zitakuweko adhabu za makosa mbali mbali ya Maadili zitakazotolewa kulingana na athari za makosa hayo kwa Chama na Umma. Halmashauri Kuu ya Taifa iliyo Msimamizi Mkuu wa Nidhamu katika Chama, itakuwa na uwezo wa kutoa hukumu zake tofauti kuzingatia mazingira yatakayokuwepo.

(2) Shabaha kubwa ya adhabu hizi ni kuwasaidia Wanachama na Viongozi kujirekebisha, ili wawe askari bora zaidi wa kutekeleza shabaha za Chama. Shabaha ya pili ni kukilinda na kukitakasa Chama dhidi ya watu, wanachama na wasiokuwa wanachama, wanadhoofisha Imani na Umoja wa Chama. Chama kisichoaminiwa kwa kauli na vitendo hakiwezi kuleta, wala kutetea Mapinduzi. Viwango vya adhabu vitakuwa:-

(i) **Onyo**
Mwanachama anayefanya kosa lisilokuwa na athari kwa Chama, na ikiwa mwanachama huyo atayakiri makosa yake na kuonyesha nia ya kutaka kujirekebisha, basi:

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 33

(a) Kamati Kuu au Kamati ya Siasa katika Ngazi inayohusika, inaweza kumpa mwanachama huyo adhabu ya Onyo.

(b) Uamuzi wa kutoa adhabu ya Onyo unaweza kutolewa katika Kikao cho chote cha Kamati ya ngazi yenye madaraka kama hayo, lakini taarifa yake itafikishwa Makao Makuu kwa kumbukumbu.

(c) Mwanachama aliyepewa adhabu ya Onyo atakuwa katika hali ya kuchunguzwa kwa muda usiopungua miezi 6, ili kumsaidia katika jitihada zake za kujirekebisha.

(d) Adhabu ya Onyo haitatangazwa hadharani.

(ii) **Onyo kali**

Mwanachama anayefanya kosa kubwa, au anayerudia kosa lile lile ambalo kwalo amekwisha pata adhabu ya Onyo bila kuonyesha nia ya kujirekebisha, basi Kamati ya Siasa inayohusika au Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, katika Ngazi inayohusika, inaweza kumpa mwanachama huyo adhabu ya Onyo Kali.

(a) Uamuzi wa kutoa adhabu ya Onyo Kali unaweza kutolewa katika Kikao cha Kamati ya Siasa ya Wilaya, au Mkoa, au Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Endapo adhabu ya onyo kali itatolewa na Kamati ya Siasa ya Wilaya au Mkoa taarifa yake itafikishwa Makao Makuu kwa kumbukumbu.

(b) Mwanachama aliyepewa adhabu ya Onyo Kali atakuwa katika hali ya kuchunguzwa kwa muda usiopungua miezi 12, ili kumsaidia katika jitihada zake za kujirekebisha.

(c) Adhabu ya Onyo Kali haitatangazwa hadharani.

(iii) **Karipio**

Mwanachama anayefanya kosa linalokipaka matope Chama, au anayerudia kosa lile lile ambalo kwalo amekwishapata adhabu ya Onyo Kali, bila ya kuonyesha nia ya kujirekebisha, basi Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa inaweza kumpa mwanachama huyo adhabu ya Karipio.

(a) Lakini tofauti na Onyo au Onyo Kali, Karipio haliwezi kutolewa kwa siri siri:litatangazwa

(b) Uamuzi wa kutoa adhabu ya Karipio unaweza kutolewa pia katika Kikao cha Kamati ya Siasa ya Mkoa au zaidi na Makao Makuu ya Chama yataweka kumbukumbu.

(c) Mwanachama aliyepewa adhabu ya Karipio atakuwa katika hali ya matazamio kwa muda usiopungua miezi 18, ili kumsaidia katika jitihada za kujirekebisha. Mwanachama akiwa katika kipindi hicho hatakuwa na haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi katika Chama; lakini atakuwa na haki ya kupiga kura kuwachagua viongozi wake wa Chama.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 35

(iv) **Kuvuliwa Uanachama**

Mwanachama atakayethibitika kuwa na tabia zilizo kinyume na Itikadi ya Chama, au ambaye ameshindwa kujirekebisha hata baada ya Karipio, lakini ambaye atayakiri makosa yake kiasi cha kuipa Kamati ya Maadili matumaini ya mwanachama huyo kujirekebisha, bado Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa inaweza kupendekeza mbele ya Kamati Kuu mwanachama huyo avuliwe haki ya kugombea katika nafasi ya uongozi.

(a) Adhabu ya kuvuliwa haki ya kugombea katika nafasi ya uongozi itatangazwa hadharani.

(b) Mwanachama atakayepewa adhabu ya kuvuliwa haki ya kugombea atakuwa katika hali ya kuchunguzwa kwa muda usiopungua miezi 24, na katika kipindi hicho atatazamiwa kutimiza Masharti na Wajibu wake wa Mwanachama, na kudhihirisha nia yake kutaka kujirekebisha.

(v) **Kuachishwa uongozi**

Kiongozi atakayekiuka Maadili ya Chama kwa kiasi cha kuvuruga uhai wa Chama, au ambaye hakuweza kujikosoa hata baada ya adhabu ya Karipio, basi Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa inaweza kupendekeza mbele ya Kamati Kuu Mwanachama huyo aachishwe uongozi. Ikiridhika, Kamati Kuu itapeleka shauri hilo mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Hivyo:-

(a) Adhabu ya mwanachama kuachishwa uongozi itatangazwa hadharani.

(b) Mwanachama atakayepewa adhabu ya kuachishwa uongozi atakuwa katika kuchunguzwa kwa muda usiopungua miezi 30, na katika kipindi hicho hicho atatazamiwa kutimiza Masharti na Wajibu wowote wa Mwanachama, na kudhihirisha nia yake ya kutaka kujirekebisha.

(vi) **Kuachishwa Uanachama**

Mwanachama anayegundulika na makosa ya Itikadi, yanayoathiri uhai wa Chama, au ambaye ameshindwa huko nyuma kujirekebisha hata baada ya adhabu ya Karipio, wala haonyeshi dalili ya kuweza kujirekebisha hata akipewa muda zaidi, basi Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa inaweza kupendekeza mbele ya Kamati Kuu mwanachama huyo aachishwe uanachama. Ikiridhika, Kamati Kuu itapeleka shauri hilo mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(a) Adhabu ya kuachishwa Uanachama itatangazwa hadharani.

(b) Mtu aliyekwisha kuachishwa uanachama hataweza kufikiriwa kwa kipindi kisichopungua miezi 36, isipokuwa kama Halmashauri Kuu ya Taifa, itaidhinisha kupunguzwa kwa muda huo.

(c) Mtu wa namna hiyo, ama aliyemaliza muda wake wa miezi 36, au aliyepunguziwa muda wa adhabu na Halmashauri Kuu ya Taifa, akitaka kuingia tena katika Chama itabidi aombe upya na maombi yake yataidhinishwa kwanza na Halmashauri Kuu ya Taifa.

(vii) **Kufukuzwa Uongozi**

Kiongozi aliyegundulika kuwa mnafiki, msaliti na mwenye kukiuka Maadili ya Chama kwa kiasi cha kuvuruga Uhai wa Chama, au ambaye hakuweza kujikosoa hata baada ya adhabu ya Karipio, basi Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa inaweza kupendekeza mbele ya Kamati Kuu mwanachama huyo afukuzwe kutoka katika uongozi wa Chama. Ikiridhika, Kamati Kuu itapeleka shauri hilo mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uamuzi wa mwisho. Hivyo:-

(a) Adhabu ya mwanachama kufukuzwa kutoka katika uongozi itatangazwa hadharani.

(b) Mwanachama atakayepewa adhabu ya kufukuzwa kutoka katika uongozi atakuwa katika hali ya kuchunguzwa kwa muda usiopungua miezi 42 na katika kipindi hicho atatazamiwa kutimiza Masharti na Wajibu wote wa Mwanachama, na kudhihirisha nia yake ya kutaka kujirekebisha.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 38

(viii) **Kufukuzwa Uanachama**

Mwanachama anayegundulika na makosa makubwa ya itikadi yanayoathiri uhai wa Chama au/na ambaye ameshindwa huko nyuma kujirekebisha hata baada ya adhabu ya Karipio, basi Kamati Kuu itapendekeza mwanachama huyo afukuzwe uanachama na itapeleka shauri hili mbele ya Halmashauri Kuu ya Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(ix) Kosa kubwa kuliko yote katika Chama Cha Mapinduzi ni kukisaliti Chama na kukiweka katika hali ama ya kushindwa katika Uchaguzi wa Dola wa ama ya kunuka mbele ya Umma; anayeshirikiana na wapinzani kuchimba na kukivuruga Chama chetu. Huyo hawezi kukubalika kuwa miongoni mwetu. Afukuzwe katika Chama. Kwa hiyo:-

(a) Ikithibitika kuwa mwanachama huyo anayatenda hayo kwa makusudi basi atakuwa amefukuzwa daima.

(b) Ikithibitika kuwa mwanachama huyo anayatenda hayo ama kwa ujinga ama kwa bahati mbaya basi adhabu yake ya kuangaliwa itakuwa miezi 48.

(c) Adhabu ya kufukuzwa uanachama itatangazwa hadharani.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 39

(3) **Rufaa**

Mwanachama au kiongozi ye yote ambaye atakuwa hakuridhishwa na adhabu iliyotolewa kwake kwa makosa ya ukiukwaji wa Maadili atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(4) **Adhabu na Muda wa Adhabu**

(i) Adhabu yo yote itakayotolewa na Kamati yenye madaraka ya kutoa adhabu atapelekewa mwenye kuadhibiwa kwa maandishi. Muda wa adhabu utakapomalizika, mwenye kuadhibiwa atapelekewa tena Taarifa ya maandishi endapo itadhihirika kuwa hakulirudia kosa lile katika kipindi alichopewa na kuwa amejirekebisha.

(ii) Lakini adhabu hiyo inaweza kupunguzwa iwapo Kamati Kuu itaridhika kuwa amejirekebisha kabla ya muda wake wa adhabu.

(5) **Kutengua adhabu**

Adhabu yo yote itakayokuwa imetolewa kuhusiana na tuhuma za ukiukaji wa Maadili haitaweza kutenguliwa na Kikao cho chote mpaka imepita miezi sita toka kutolewa kwake.

UTARATIBU WA KUENDESHAJI VIKAO

9. (1) Vikao vya chama vina kazi muhimu sana ya kujenga itikadi moja katika Chama. Vikao ni uhai kwa

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 40

kuwa:

(i) Vikao vinafanya maamuzi ya pamoja yanayowabana wote.

(ii) Vikao ni vyombo vinavyotoa nafasi ya kukosoa na kukosoana katika nadharia na Itikadi ya Chama, vinavyosaidia ufafanuzi wa sera na siasa ya Chama juu ya masuala mbalimbali.

(iii) Vikao ndivyo vinavyowezesha wanachama na pia viongozi kujua wenzao wanafikiri nini juu ya masuala mbalimbali; ndivyo vinavyoyajenga mawazo hayo kwa mjadala, hadi kufikia uamuzi mmoja. Bila Vikao hakuna Uongozi mmoja, na kwa kweli hakuna Chama.

(iv) Kwa hiyo vikao ni vyombo vya kuimarisha Mshikamano katika Itikadi na Nadharia ya Chama.

(v) Kazi moja itakayopewa umuhimu ni kuimarisha Uongozi wa Vikao, ili viweze kutimiza jukumu hili la kujenga Itikadi moja.

(2) Kazi ya msingi na muhimu katika kujenga Uongozi mmoja katika Chama ni kutekeleza kwa dhati Kanuni ya Demokrasia na Nidhamu ndani ya Chama.

(i) Chama chetu lazima kiendeshwe kwa misingi ya Demokrasia katika kila Ngazi. Wajumbe wa vikao lazima wawe sawa na huru katika kujadili

masuala ya mikutano yao. Uhuru huu uheshimu maoni ya wachache lakini usiathiri Kanuni ya “wengi wape”

(ii) Maana lazima mjadala ufike mwisho;na Chama ni chombo cha kutenda, na kutenda kama kitu kimoja. Basi lazima kuwepo nidhamu ndani ya Chama. Kwanza nidhamu ni kukubali kuwajibika kwa maamuzi ya vikao vinayowahusu;na pili ni kwa Vikao vya Chini na wanachama wake kutii maamuzi ya vikao vya juu yao. Mwalimu amewahi kusisitiza “Nidhamu bila Demokrasia ni Udikteta na Demokrasia bila Nidhamu ni Fujo”.

(iii) Kanuni ya Demokrasia ni Nidhamu ndiyo inayokiwezesha Chama kuwa cha kidemokrasia, na papo hapo kuwa chombo cha kuongoza mapinduzi kutokana na nidhamu yake inayokipa uongozi mmoja katika vitendo.

(3) Ukiacha haki zake za Uraia, Mwanachama wa CCM anayo “haki ya kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya CCM, pale ambapo anahusika. Lakini vile vile mwanachama anaagizwa na Katiba ya Chama kutimiza Masharti ya Uanachama wa kutambua kuwa Nguvu za Chama chetu ni Umoja.

(4) **Wajibu wa Mwenyekiti**

Mwenyekiti wa kikao atakuwa na wajibu mkubwa wa kusimamia Katiba na haki za kila Mjumbe wakati akiongoza kikao hicho. Katika kutekeleza hayo atapaswa kutenda mambo yafuatayo:-

(i) Kuzingatia hoja zinazotolewa, na aweze kuzieleza kwa wakati atakapofanya majumlisho ya hoja zote zilizozungumzwa.

(ii) Kutoa nafasi sawa kwa Wajumbe, kuzingatia hoja zilizowasilishwa katika kikao, kulingana na utaratibu uliotolewa.

(iii) Kusimamia Nidhamu na Maadili kwa wajumbe wote majadiliano yanapofanyika, ili kudumisha mazingira ya amani na utulivu.

(5) **Utaratibu wa kuendesha mazungumzo**

(i) Mjumbe atapata nafasi ya kuzungumza baada ya kuruhusiwa na Mwenyekiti. Akishapata ruhusa hiyo atasimama na kuzungumza hadi atakapomaliza, kulingana na muda uliowekwa.

(ii) Wakati wote atakapokuwa anazungumza, Mjumbe atakuwa amesimama mahali pake, isipokuwa kama Mwenyekiti ameruhusu vinginevyo kama, kwa mfano, kuna chombo cha kuzungumzia, atakwenda kwenye eneo kilipo chombo hicho. Wakati wote ataelekeza mazungumzo yake kwa Mwenyekiti wa Kikao.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 43

(iii) Endapo Mjumbe anadhani anayo hoja muhimu ambayo angependa izungumzwe na Kikao, lakini haipo kwenye Agenda za Kikao, ataomba iwekwe kwenye Orodha ya Mengineyo; lakini uamuzi wa Mwenyekiti katika hilo ni wa mwisho.

(6) **Yanayoruhusiwa kuzungumzwa**

(i) Mjumbe atapaswa kuzungumzia hoja ile tu itakayokuwa imewasilishwa kwenye Kikao, na hataruhusiwa kurudia rudia maelezo ama yake ama yaliyokwisha zungumzwa na Wajumbe wengine.

(ii) Maelezo yatakayokuwa yanatolewa na Mjumbe yanapaswa kuwa ya uhakika na sahihi, ambayo anaweza kuyatolea uthibitisho endapo atatakiwa na kikao kufanya hivyo.

(iii) Mjumbe ataruhusiwa kutoa maelezo yake kwa muda utakaokuwa umepangwa lakini Mwenyekiti ataweza kumruhusu kuendelea zaidi ya muda huo, iwapo ataona maelezo yake ni muhimu kwa kikao.

(iv) Mjumbe ambaye ameshatoa maelezo yake juu ya hoja inayojadiliwa anaweza, kwa ruhusa ya Mwenyekiti, kupata nafasi tena ya kufanya mabadiliko katika maelezo yake aliyoyatoa hapo awali iwapo atakuwa amepata hoja yenye nguvu zaidi kuliko aliyotoa kwanza.

(v) Mjumbe aliyetoa hoja ya msingi au hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika hoja iliyokwisha kutolewa anaweza, kwa ruhusa ya Mwenyekiti, kupewa ruhusa ya kujibu kabla uamuzi haujatolewa kwa hoja hiyo, bila kuongeza maelezo mengine ambayo hayakuchangiwa na wajumbe.

(7) **Taarifa**

(i) Kwa Taarifa (Point of information)

Mjumbe anaweza kuingilia kati hotuba ya Mjumbe mwingine, kwa ruhusa ya Mwenyekiti, iwapo ana habari muhimu ambayo anadhani ina manufaa kwa kikao, kama akiitaja. Mwenyekiti atakuwa na hiyari ama kuikubali taarifa ama kuikataa, na hata kumketisha chini huyo mwenye taarifa au msemaji wa awali.

(ii) Nje ya Mstari (Point of Order)

Mjumbe anaweza kuingilia kati hotuba ya Mjumbe mwingine kumkumbusha Mwenyekiti kuwa Mjumbe anayezungumza ametoka nje ya agenda iliyoruhusiwa. Mjumbe atalazimika kueleza kwa nini anafikiri hivyo. Mwenyekiti atasikiliza hoja hiyo na akiikubali, basi atamketisha Mjumbe aliyeingilia kati. Namna nyingine atamruhusu aliyetoka nje ya mstari. Basi Mwenyekiti aikatae hoja. Mjumbe aendelee na hotuba yake.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 45

(iii) Utaratibu (Point of Procedure)
Mjumbe anaweza kuingilia kati hotuba ya Mjumbe mwingine iwapo anahisi kuwa Kikao kinaendeshwa kinyume na utaratibu. Hoja hiyo haihusu maudhui ya mazungumzo ya Mjumbe aliyekuwa ameruhusiwa. Mwenyekiti akiridhika na hoja hiyo basi atamuomba radhi Mjumbe aliyekuwa anazungumza na kurekebisha hali hiyo kwa kurudi kwenye utaratibu.

(8) **Kukatizwa kwa mazungumzo ya Mjumbe**

(i) Mjumbe aliyepewa nafasi ya kuzungumza ataweza kukatizwa mazungumzo yake iwapo kutatokea yafuatayo:-

(a) Mwenyekiti ataamua kuzungumza kwanza ili kuelekeza majadiliano yaende vizuri.

(b) Mjumbe mwingine ataruhusiwa kutoa Taarifa ya Ufahamisho ya nje ya Mstari au Utaratibu.

(c) Mjumbe ataonyesha kurudia rudia maelezo yake, ama kutoa maelezo yasiyohusiana na Hoja inayojadiliwa.

(d) Mjumbe katika maelezo yake atakuwa anakiuka mambo yanayokatazwa na Kanuni hizi.

(e) Mjumbe akiridhika kwamba Hoja inayojadiliwa imejadiliwa vya kutosha, ataweza kumuomba Mwenyekiti wa Kikao kukatiza majadiliano.

(9) **Mambo yanayokatazwa wakati wa Kikao**

(i) Kutumia maneno au maelezo yanayoashiria kutukana dini, jinsia, rangi au ukabila.

(ii) Kutumia “maneno machafu”.

(iii) Kutumia maneno ya uchochezi kwa Wajumbe ili waasi Chama ama Serikali.

(iv) Kutumia maneno ya matusi, vitisho, maudhi, kejeli, kwa Mjumbe mwingine ye yote au kwa Viongozi wa Chama na Serikali.

(v) Kutumia maneno ya kashfa kwa mjumbe ye yote au kwa viongozi wa Chama na Serikali.

(vi) Kutumia maneno au maelezo ya kudhalilisha utu wa Mjumbe ye yote au wa kiongozi wa Chama kwa kisingizio cha kutumia nafasi yake ya kukosoa.

(vii) Kutumia maneno ya kudhihaki Viongozi wa Chama au Serikali kwa lengo la kuushawishi Mkutano ukubaliane na Hoja zake.

(viii) Kutoa maelezo yanayofichua siri za Chama au Serikali ambazo hazitakiwi kujulikana katika kikao hicho.

(ix) Kutumia vifaa vya kunasia mazungumzo ya kikao, kwa ajili ya matumizi binafsi au kwa

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 47

matumizi ya Vyombo vya Habari, isipokuwa kama imeruhusiwa kwa maslahi ya Chama tu.

(x) Kurushiana maneno Mjumbe na Mjumbe mwingine, kusoma gazeti au Makala isiyohusiana na Hoja inayojadiliwa, wakati Mjumbe mwingine anatoa maelezo yake.

(xi) Kuzungumza jambo lo lote ambalo limeundiwa Kamati au Tume ila anaweza kuomba Taarifa iwasilishwe mapema iwapo ataona kuwa muda uliotolewa kwa kazi hiyo umepita.

(xi) Ni muhimu wajumbe wote kuonyesha mwenendo mzuri ambao utatoa ushirikiano utakaoweza kumsaidia Mwenyekiti kuendesha kwa utulivu na amani majadiliano ya Kikao na kufikia uamuzi katika muda uliowekwa wa Kikao hicho. Ni muhimu kwa kila Mjumbe kuzingatia haki zake na utaratibu wa kuendesha vikao vya chama kwa mujibu wa Kanuni hizi.

KUBADILI KANUNI

10. Halmashauri Kuu ya Taifa itakuwa na haki ya kubadili vifungu vyo vyote vya Kanuni hizi, ama kutokana na ushauri wa Kamati Kuu ama kutokana na ushauri mwingine, kulingana na uzoefu utakaopatikana katika utendaji kazi wa Kamati ya Usalama na Maadili Taifa.

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 48

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 49

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 50

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 51

KANUNI ZA UONGOZI:Layout 1 6/2/10 4:01 PM Page 52